JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MAUDHUI NA. 05/Sep/2019/2020**

**DHIDI YA**

**KWANZA ONLINE TV**

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA YA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA MITANDAONI), 2018.**

## 1.0 UTANGULIZI

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa leseni ya kutoa huduma za utangazaji kwa Kwanza Online TV, kwa ajili ya kuchapisha na kutangaza habari mbali mbali mtandaoni.

1.2 Kwa mujibu wa Kanuni ya 4 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu la kutunza kumbukumbu za watoa huduma wote wa maudhui mtandaoni pamoja na kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya mtoa huduma yoyote wa maudhui mitandaoni atakayekiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni au sheria nyingine.

1.3 Tarehe 13 Septemba, 2019, Kwanza Online Television kupitia chaneli yake walirusha taarifa isiyo na usahihi na ukamilifu wa majina ikilenga kupotosha jamii kuhusu, mtu ambaye habari hiyo ilikuwa inamhusu, kinyume *na Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018,* ikisomwa pamoja na *Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Redio na Televisheni), 2018,* ambazo zinamtaka mmiliki wa chombo cha habari mtandaoni kuzingatia weledi na maadili ya uandishi wa habari katika kuweka maudhui mtandaoni na kuhakikisha maudhui yake hayaleti usumbufu au mkanganiko au upotoshaji kwa jamii au mlaji wa maudhui hayo.

1.4 **Kwanza Online TV**, waliweka taarifa ya picha jongefu kwenye chaneli yao ya mtandao wa kijamii wa Facebook yenye kichwa cha habari ***"Gwajima apata ajali, dereva wake amuokoa.***" ambapo ***Mtangazaji wa Kwanza Online TV alisikika akisema***... *"Tukio hilo limetokea*

*Septembea 11 mwaka huu majira ya saa moja wakati dereva wa gari hilo lenye namba za usajili STL 5978 akijiandaa kuanza safari mara moja baada ya Dokta Gwajima kuhitimisha mazungumzo na wakazi wa kata ya Nanguruwe waliojitokeza kutoa kero zao kuhusu kituo hicho cha afya.*

Dereva wa gari hilo Seif Bakari ameeleza *kuwa aliona moshi ukitoka kwenye usukani na baadae kuuchunguza ndipo akabaini kwa kuona moto unatoka kwenye injini ambapo wakati anauzima moto huo Dokta Gwajima akaingia ndani ya gari bila kujua.....akizungumzia tukio hilo Dokta Gwajima alisema kuwa ni mapenzi ya Mungu kunusurika katika ajali hiyo huku wananchi waliojitokeza kuuzima moto huo wakazungumzia namna walivyouzima moto huo..."*

1.5 Kitendo cha kurusha taarifa isiyo na usahihi na ukamilifu wa majina huku ikilenga kupotosha jamii kuhusu, mtu ambaye habari ilikuwa inamhusu. **Kwanza Online TV** imekiuka Kanuni Na. 7(1)(a) & (b) Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018, ikisomwa pamoja na Kanuni Namba15 (2) (b) (c) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Redio na Televisheni), 2018.

> *7(1) A licencee of online radio and television intended for broadcasting over the public internet with the objective of informing, entertaining and educating the public shall adhere to the following conditions:*
>
> *(a) content streamed to abide to regulations governing the broadcasting services;*
> *(b) adhere to journalism ethics and professionalism;*
>
> *15(2). The licensee shall-*
> *(b) report accurately, impartially, fairly and in a non-partisan manner;*
> *(c) report news in an objective and balanced manner, without intentional or negligent departure from the facts, whether by distortion, exaggeration, misrepresentation or material omission.;*

1.6 Vile vile, **Kwanza Online TV** wamekuwa wakirusha na kuonesha taarifa mbalimbali bila ya kuwa ama kuchapisha Sera au Miongozo ya watumiaji (Online Policy or Guidelines) kinyume na *Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018* ambazo zinamtaka mmiliki wa mtandao azingatie kuwa na sera au mwongozo ambao utamsaidia mtumiaji kuonyesha uwajibikaji wakati anapotumia huduma za mawasiliano.

1.7 Kitendo cha kurusha na kuonesha taarifa mbalimbali bila ya kuwa ama kuchapisha Sera au Miongozo ya watumiaji (Online Policy or Guidelines) **Kwanza Online TV** imekiuka Kanuni Na. 5 (1) (c) za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018. Kanuni tajwa zinasomeka kama ifuatavyo;

> *5.-(1) For the purpose of these Regulations, an online content provider shall have the obligations to-*
>
> *(c) establish online policy or guideline and make it available to users*

## 2.0 WITO WA KUFIKA MBELE YA KAMATI YA MAUDHUI

Tarehe 25 Septemba, 2019, Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa **Kwanza Online TV**, wito wa kufika mbele ya Kamati kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria.

Tarehe 26 Septemba, 2019, saa 04:30 asubuhi, uongozi wa **Kwanza Online TV** ukiongozwa na Bi. Maria Sarungi Tsehai, Mtendaji Mkuu na Mkurugenzi wa **Kwanza Online TV** na Bw. Mashaka Mgeta Mhariri wa Vipindi ulifika mbele ya Kamati ya Maudhui kwa ajili ya kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria.

## 3.0 KUSIKILIZA NA KUANGALIA MAUDHUI MTANDAONI YA KWANZA ONLINE TV YA TAREHE 26 SEPTEMBA, 2019

Kamati ya Maudhui na Uongozi wa **Kwanza Online TV** walisikiliza na kuangalia maudhui mtandaoni ya tarehe 13 Septemba, 2019 yaliyochapishwa na **Kwanza Online TV** katika chaneli yao mtandaoni ili kujiridhisha iwapo maudhui hayo yalikiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni.

## 4.0 MAELEZO YA UTETEZI YA KWANZA ONLINE TV

Katika utetezi wao wa maandishi, Uongozi wa **Kwanza Online TV**, ukiongozwa na Bi. Maria Sarungi, ulikana kukiuka Kanuni yo yote na kusema kuwa katika kutangaza tukio hilo walizingatia weledi na maadili ya uandishi wa habari kwakuwa mtangazaji wao alionesha tukio lenyewe la moto wakati gari likiungua, pia walidai kuwa kulikuwepo na ushahidi wa sauti na video kutoka kwa muathiriwa wa tukio la ajali hiyo ambaye ni Dkt. Gwajima na dereva wake, na vilevile kulikuwa na ushahidi wa mashuhuda wawili wa tukio hilo waliohojiwa.

Waliendelea kuieleza Kamati kuwa **Kwanza Online TV** ilikwenda mbali zaidi kwa kuonesha mwendelezo wa habari hiyo jinsi Dkt. Gwajima alivyoendelea na kazi zake kama kawaida. Uongozi wa **Kwanza Online TV** ulisisitiza kuwa taarifa yao haikuwa na lengo la kupotosha, kukuza au kudanganya.

Pamoja na utetezi wao wa maandishi, **Kwanza Online TV** waliendelea kueleza yafuatayo:-

**Bw. Mashaka Mgeta** aliendelea kusisitiza kutokiuka Kanuni yo yote na kusema alipoipata taarifa hiyo alitaka kujiridhisha na kubaini kama ni habari inayokidhi vigezo na alijiridhisha kama ni habari wakati kiongozi wa Serikali, Dkt. Gwajima alikuwa kwenye ziara ya kikazi katika kutekeleza majukumu yake ndipo ajali hiyo ilipotokea ambapo wao waliipima na kuona ni tukio la kuhabarisha umma.

Aliendelea kuiambia Kamati kuwa, ili kuthibitisha kwamba kulikuwa na ajali na taarifa hiyo ni ya kweli, walimtaka mwandishi wa kituo chao

kuchukua jitihada ya kumuhoji dereva wa gari pamoja na Dkt. Gwajima mwenyewe, na baadaye walikwenda kuwahoji watu walioshuhudia tukio hilo.

Vile vile, Bw. Mgeta alisema mwandishi wao aliendelea kuifuatilia habari hiyo na kubaini kuwa Dkt. Gwajima alikuwa akiendelea na majukumu yake kama kawaida. Vile vile aliendelea kusisitiza kwamba habari hiyo ilikuwa na umuhimu na ilikidhi vigezo vyote vya habari na haikuwa na upotoshaji wo wote wala mapungufu yo yote.

Bw. Mgeta alisema kwamba kituo chao kinatoa habari zake kupitia mitandao ya kijamii kama vile YouTube na Facebook, ambapo kina utaratibu wa kunakiri taarifa mbali mbali na kuzirusha katika mitandao hiyo.

Bi. Maria Sarungi aliomba kupewa fursa ya kuonesha taarifa hiyo ya Facebook na kusema kuwa haikuwa na upotoshaji wa jina au taarifa kwa sababu katika mtandao wa Facebook kuna ukomo wa idadi ya maneno ya kuchapisha. Hivyo wao waliweka utangulizi wa mwanzo ambao ulitaja kikamilifu majina na cheo cha Dkt. Gwajima.

Alisema halikuwa lengo lao kufanya upotoshaji na taarifa yao ilikuwa inakidhi vigezo vya habari, vigezo vya TCRA na vigezo ya Kimataifa.

Kuhusu tuhuma za Kwanza TV Online kurusha na kuonesha taarifa mbali mbali bila ya kuwa na ama kuchapisha Sera au Miongozo ya watumiaji (Online Policy or Guidelines), ni kinyume na Kanuni Na. 5 (1) (c) za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018.

Bi. Sarungi alisema si kweli kwamba wao hawana Sera na kudai kuwa kituo chao kina Sera ya Uhariri pamoja na Sera ya watumiaji na mtu ye yote akiihitaji awaweza kuipata muda wo wote kwani Sera yao inatoa nafasi kwa watumiaji kuwasiliana na kituo chao wakati wowote.

Kuhusu kutochapisha Sera hiyo alisema kuwa kwa mujibu wa Kanuni Na. 5 (1) (c) ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018, wao walisema wanavyoielewa hiyo Kanuni ni kwamba mtoa huduma wa maudhui mtandaoni anatakiwa kuwa sera na kuweza kumpa mtumiaji pale inapohitajika. Aliongeza kuwa Kanuni hazisemi kuwa lazima Sera ichapishwe. Aliongeza kusema kuwa kwenye mtandao wa YouTube, Sera yao haina “option” ya kuweka Sera binafsi za “subscribers” wa mtandao huo, hivyo wasingeweza kuchapisha katika chaneli yao ya YouTube.

Katika kujumuisha utetezi wake, Bi. Maria Sarungi alisema kwamba **Kwanza Online TV** imejikita kutoa maudhui yenye ubora na wamewekeza kwa watendaji na wanafuata kanuni na vigezo vyote. Alisema hawajakiuka Kanuni yo yote na kwamba hakuna mwonekano wa kuvunja Kanuni yo yote.

## 5.0 TATHMINI YA KAMATI

Kamati ya Maudhui imebaini kwamba **Kwanza Online TV** imechapisha maudhui yenye lengo la kupotosha hasa kwa kutokuzingatia miiko na misingi ya maadili ya uandishi na utangazaji wa habari unaomtaka mwandishi azingatie usahihi wa majina katika habari husika (*material omission).* Hoja ya kuwa, katika picha jongefu kwenye ukurasa wa *Facebook*, jina na cheo viko kikamilifu pale chini ni hoja dhaifu kwa kuwa, kwa vyovyote vile, habari katika picha jongefu inatakiwa kujitosheleza. Kwa uwasilishaji huo, ni vigumu kwa mtu ambaye hatasoma, kama vile mtu mwenye ulemavu wa kuona, kupata usahihi ni Gwajima yupi anayezungumziwa katika tukio hilo.

Pamoja na utetezi kuwa habari iliyowekwa *Facebook* ilikuwa na maelezo juu ya Dkt. Gwajima, taarifa yenyewe katika picha hiyo iliondolewa sehemu ya awali ya utambulisho wa majina kamili ya Dkt.Gwajima na badala yake taarifa iliendelea kutaja tu "Dkt. Gwajima" katika habari nzima badala ya jina kamili "Dkt.Dorothy Gwajima" jambo mbalo, kwa mtazamaji wa kawaida wa habari ile ni vigumu kufahamu ni Gwajima yupi. Zaidi, kwa kuwa jina Gwajima, katika jamii kwa sasa hivi limekuwa maarufu kwa kumuhusisha Gwajima mbaye ni Mchungaji, taarifa hiyo imepotosha umma kwani mtazamaji anaposikia "Dkt. Gwajima Apata Ajali" kinachomjia haraka ni Gwajima anayefaahmika na kuvuma zaidi katika jamii.

Pia, matumizi ya neno "ajali" katika habari hiyo, hayakuakisi usahihi wa tukio lenyewe kulingana na uhalisia wa kilichotokea. Katika taarifa hiyo, jinsi neno hili lilivyotumika na picha inavyooneka inadhihirisha dhahiri kuwa tukio hilo limekuzwa kwa makusudi.

Hivyo, ni tathmini ya Kamati kuwa kwa kutumia jina Gwajima peke yake na kwa namna walivyotumia neno ajali katika habari hiyo, ililenga kukuza habari hiyo kwa kuleta mvuto kwa jamii (news sensation).

Juu ya tuhuma za kutokuwa na/kutochapisha Sera au Miongozo ya watumiaji (Online Policy or Guidelines) kinyume na Kanuni Na. 5 (1) (c) za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018, Kwanza Online TV imeieleza Kamati kuwa uelewa wao ni kuwa Sera hiyo walitakiwa kuwa nayo tu na kumpa mtumiaji inapohitajika. Kwa mujibu wa Kanuni tajwa, **Kwanza Online TV** ilitakiwa kuwa na Sera hiyo na kuhakikisha kuwa Sera hiyo inapatikana kwa watumiaji wa maudhui yao, ili kila mtumiaji wa maudhiui hayo ajue ni nini Sera ya **Kwanza Online TV** katika matumizi sahihi na salama ya mitandao. Kuwa na Sera hiyo na kuiweka kabatini haikidhi matakwa ya Kanuni tajwa kwani Kanuni inasema wawe na Sera hiyo na iwe "available" kwa watumiaji. "*Make it available to users*". Hivyo, Kamati imejiridhisha kuwa **Kwanza Online TV** imekiuka Kanuni Na. 5 (1) (c) ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018.

## 6.0 UAMUZI WA KAMATI

Baada ya kusikiliza na kutafakari kwa kina maelezo ya utetezi yaliyotolewa na Uongozi wa **Kwanza Online TV**, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa, **Kwanza Online TV,** kupitia chaneli yake mtandaoni imekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mitandaoni), 2018.

Hivyo, kwa mujibu wa Kifungu cha 28 (1) (b) na (d) cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172, Marejeo ya Mwaka 2017, Kamati ya Maudhui imeamua kuifungia **Kwanza Online TV** kutoa huduma kwa kipindi cha miezi sita (6) kwa ukiukaji wa Kanuni kama ilivyoainishwa katika shauri hili, ili waweze kujirekebisha. Kamati imefikia uamuzi huu kwa lengo la kuwapa fursa **Kwanza Online TV** kujitambua, kujitafakari na kujipanga vizuri zaidi ili waweze kuendesha kituo chao kwa kuzingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na taaluma ya habari na utangazaji.

Uamuzi huu umetolewa na kusomwa **Dar es Salaam**, leo tarehe **27** mwezi **Septemba** mwaka **2019**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia leo.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Bw. Joseph Method Mapunda**

..............................................................................

**Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S.L.P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

**PAMOJA NA WAJUMBE WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Bw. Abdul Ramadhani Ngarawa**......................................
2. **Bw. Derek Kaitira Murusuri**.........................................
3. **Bw. Jacob Gregory Tesha**............................................